

2



WAKATI WA TUKIO

- **Vaa uhusika** ikiwemo matumizi ya lugha sahihi na mavazi yanayoonyesha heshima.
- **Mwandae mwakilishi** wa uongozi kukutambulisha na kutoa utangulizi kuhusu kikao.
- **Wasilisha mada** kwa kusisitiza taarifa muhimu kama faida na athari ndogo ndogo za tohara, mahali na muda wa huduma, umri wa walengwa na gharama ya huduma.
- **Ruhusu muda wa majadiliano**, maswali na maazimio kwa kuwashirikisha viongozi na mwakilishi kutoa ufafanuzi inapohitajika. Jibu mitazamo potofu ikijitokeza.
- **Toa shukrani** kwa mamlaka husika, mwakilishi wa uongozi na viongozi walioshiriki na watajije namba yako ya simu iwapo watahitaji kufanya mawasiliano baadaye.
- **Kamilisha taratibu za kiofisi** kama kujaza fomu ya mahudhurio na wajulishe washiriki kuwa utasubiri iwapo kuna mshiriki anataka kuwa na maongezi binafsi na wewe.

3



BAADA YA TUKIO

- **Wasilisha muhtasari wa kikao** kwa mamlaka iliyoidhinisha kikao na viongozi wako kwa taarifa na msaada katika kufanyia kazi maoni, maazimio na changamoto.
- **Fuatilia maazimio ya kikao** kupitia mamlaka husika, ofisi za washiriki, simu za mkononi na kukutana ana kwa ana wa wahusika.
- **Jenga ukaribu** na viongozi rafiki na mwakilishi kuhakikisha mwendelezo wa ushirikiano.
- **Tumia majukwaa ya viongozi** mfano mikutano ya kijiji, kamati za maendeleo, kamati za UKIMWI na sherehe/maadhimisho ya kitaifa kuhimiza viongozi kuunga mkono huduma ya tohara.

NI MUHIMU

- Kuomba idhini ili kupata fursa ya kuyafikia makundi mbalimbali ndani ya jamii.
- Kutambua mazingira na mahitaji ya wahusika ili kupunguza au kuondoa changamoto.
- Kuwa makini katika matumizi ya lugha na kuheshimu miiko ya kundi husika.
- Kutoa shukrani kwa viongozi, wawakilishi na washiriki wote katika vikao.
- Kushauriana na viongozi wako katika hatua zote kwa taarifa na msaada unapohitajika.

ANGALIZO

Uwe mwangalifu katika kuchagua viongozi wa kata ambao utashirikiana nao. Hususan kuhusu itikadi zao za kisiasa na kidini. Hakikisha mchanganyiko wa wawakilishi bila kwegemea upande wowote ama kutilia mkazo itikadi yoyote. Hii itaepusha kuchochea mitazamo potofu juu ya huduma. Shauriana na mamlaka husika na viongozi wako.

VYANZO VINGINE VYA KUJENGA UZOEFU KATIKA MADA

- Machapisho ya uhamasishaji wa huduma ya tohara.
- Ufafanuzi wa utekelezaji kutoka kwa viongozi wako.
- Ushauri wa kitaalamu kutoka kwa watoa huduma ya tohara.
- Taarifa za serikali kuhusu tohara, UKIMWI na saratani.

